HAKUNA MALIPO YASIYOFAA HAKUNA MANUFAA YASIYOFAA

Hakuna malipo ya pesa au kitu chochote kilicho na thamani kinaweza kutolewa, kuahidiwa au kulipwa, moja kwa moja au kwa njia nyingine ile, kwa mtu yoyote, ikiwa ni pamoja na maafisa wa serikali, ili upokee manufaa yasiyofaa. Hii ni pamoja na kupeana zawadi au kumlipia afisa usafiri na ukarimu bila idhini ya kabla kutoka kwa Universal.

Kwa mfano, hatutoi malipo:

- Kwa afisa ili tupate mauzo
- Kwa afisa ili tushawishi utengenezaji sheria
- Kwa mchunguzi ili apitishe uchunguzi
- Kwa afisa wa Forodha ili aharikishe makaratasi
- Kwa afisa ili aratibu uchunguzi wa bidhaa wa kabla ya kusafirishwa
- Kwa afisa ili atoe cheti cha kupokea bidhaa
- Kwa afisa wa Forodha ili achakate visa au kibali cha kazi
- Kwa afisa ili tupate cheti cha afya ya mimea
- Kwa afisa kushawishi wakaguzi wa kupima ubora
- Kwa afisa yoyote kama bahshishi au kiinua mgongo kwa kufanya kazi yao

HAKUNA MALIPO YATAFANYWA KWA NIABA YA UNIVERSAL. MALIPO HAYO YAKIITISHWA, TUJULISHE MARA MOJA.

Tunatarajia yafuatayo kutoka kwako:

- Usichukue hatua ambazo zitakiuka sera za Universal, FCPA au sheria nchini mwako.
- Tambua na utii Kanuni za Maadili za Universal na Mwongozo wa Uzingatiaji wa Kupambana na Ufisadi.
- Tujulishe kama mtu yoyote kati ya maafisa, wakurugenzi au wafanyikazi wako ni maafisa wa serikali, jamaa wa afisa au kama afisa ako na manufaa yoyote ya kifedha katika shirika lako.
- Usitumie makontrakta wadogo, wawakilishi au maajenti wa akaunti yetu bila idhini ya kabla iliyoandikwa kutoka kwa Universal.
- Tushauri mara moja pakiwa na mabadiliko yoyote muhimu katika shirika lako yanayoweza kuathiri uzingatiaji kama vile kubadilika kwa umiliki au usimamizi.
- Tujulishe kama afisa wa serikali atawahi kukuitisha malipo au uwapatie kitu kinachokiuka sera za Universal.

Universal
UNIVERSAL CORPORATION

P.O. Box 25099
Richmond, Virginia 23260
USA

www.universalcorp.com
E-mail: compliance@universalleaf.com
www.Ethicspoint.com

LEG1302 SWA

Universal
UNIVERSAL CORPORATION

MAADILI YA UNIVERSAL: KUONGOZA KWA UADILIFU

KUPAMBANA NA UFISADI

www.universalcorp.com/compliance

Universal
UNIVERSAL CORPORATE COMPLIANCE

KUONGOZA KWA UADILIFU

George Freeman
Mwenyekiti, Rais, na Afisa Mkuu Mtendaji

Familia ya makampuni ya Shirika la Universal imekuwa ikifanya biashara kwa zaidi ya miaka 100. Kwa wakati huo, watu wetu duniani kote wamejitahidi kuunda na kulinda raslimali yetu muhimu zaidi-uadilifu. Ufisadi ni tisho kwa biashara na wafanyikazi wetu, na ni kinyume na utamaduni wetu. Ni wajibu wetu kwa wateja wetu, jumuiya zetu, washikadau wetu, na kwetu sisi wenyewe kufanya biashara yetu kwa kufuata viwango vya juu vya kimaadili na kukataa ufisadi. Kusema kwa urahisi: ***Huwa hatulipi rushwa***.

Tunajichukulia kama watu walio na viwango vya juu na tunatarajia wabia wetu wa biashara duniani kote wajichukulie vivyohivyo. Ukiwa mgawaji, mchuuzi, ajenti, msafirisha mizigo, dalali, mshauri, au mshenga, tunatarajia ushiriki maadili yetu na kujitolea kwetu kwa uzingatiaji wa kisheria.

Haijalishi ulipo duniani au aina ya huduma unayotoa kwa Universal, haikubaliki kamwe kutoa rushwa, bahashishi, au malipo yasiyofaa ya aina yoyote ile kwa mtu yoyote.

Tunahitaji ujitolee kufuata sera zetu. Kufanya kitu kinachofaa na kudumisha uhusiano wenye uaminifu na sisi kutasaidia kujenga msingi thabiti wa kuunda mazingira mazuri ya kazi yalivyo yanavyotakikana na uhusiano endelevu wa biashara unaonufaisha pande zote mbili.

PROGRAMU YA UZINGATIAJI YA UNIVERSAL KWA JUMLA

Universal
UNIVERSAL CORPORATE COMPLIANCE

Programu ya Uzingatiaji ya Universal kwa Jumla inahakikisha tunatenda kwa uadilifu, kulingana na sera zetu za uzingatiaji, Universal imeanzisha ukurasa wa Uzingatiaji kwenye tovuti yake inayopatikana kwa umma, na inadumisha ukurasa huo wa Uzingatiaji kwa lugha kumi na tano.

Tafadhali tembelea ukurasa wetu wa Uzingatiaji kwa maelezo zaidi kuhusu uzingatiaji:
www.universalcorp.com/compliance

KANUNI ZA MAADILI NA MWONGOZO WA UZINGATIAJI WA KUPAMBANA NA UFISADI

Universal huthamini uzingatiaji na uadilifu. Sehemu muhimu ya mafanikio yetu ni kwa sababu ya kujitolea kwetu kwa uadilifu. Kanuni za Maadili za Universal (Code of Conduct (CoC)) na Mwongozo wa Uzingatiaji wa Kupambana na Ufisadi (Anti-Corruption Compliance Manual (ACM)) ni hati zetu muhimu zaidi za uzingatiaji na maadili, na zinataja sera zetu nyingi zinazohusu uzingatiaji.

SHERIA YA VITENDO VYA UFISADI VYA UGENINI YA MAREKANI (FCPA)

"Hakuna mtu anayetoa, mwananchi, aliye na kiungo cha Marekani anaweza kuchukua hatua kiufisadi kuendeleza malipo au ahadi, kutoa, au udhinisho wa malipo ya ufisadi au kitu chochote cha thamani moja kwa moja au kwa njia nyingine ile ("akijua") kwa afisa wa kigeni ili apate au adumishe biashara au manufaa yasiyofaa."

Universal hutii FCPA na tunatarajia wabia wetu wa biashara duniani kote waitii pia. FCPA inafanya ***kuwa kinyume na sheria kulipa au kuahidi kulipa pesa au kupeana kitu chochote cha thamani*** kwa afisa wa serikali ili kuongeza biashara au kudumisha biashara au kupata manufaa yoyote yasiyofaa. Hii inahusu malipo na zawadi zilizopeanwa na makampuni na wafanyikazi wao, na pia mshiriki wa tatu anayewakilisha makampuni hayo. Programu ya Uzingatiaji ya Universal kwa Jumla na sera zetu hutusaidia kutii FCPA. Hiyo ndio sababu tunakuhitaji ujitolee kufuata sera zetu.

FCPA inakataza "afisa" ajumuishe: afisa au mfanyikazi yoyote wa serikali ya kigeni au idara, uajenti wowote, au wakala wake, au wa shirika la umma la kimataifa, au mtu yoyote anayetenda katika uwezo wa afisa kwa au kwa niaba ya serikali yoyote au idara, uajenti, au wakala wowote kama huo, au kwa niaba ya shirika la umma la kimataifa kama hilo.

Tafadhali angalia ukurasa 8 wa ACM kwa maelezo zaidi.